# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO ZANZIBAR NAMBA 8 YA MWAKA 2012 NA KUTUNGA SHERIA YA TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI


1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.


### SEHEMU YA PILI
### KUANZISHWA KWA TAASISI


3. Kuanzishwa kwa Taasisi.
4. Muhuri na nembo ya Taasisi.
5. Kazi za Taasisi.


### SEHEMU YA TATU
### UONGOZI WA TAASISI


6. Uanzishaji na Muundo wa Bodi.
7. Katibu wa Bodi.
8. Kazi za Bodi.
9. Uwezo wa Bodi.
10. Muda wa wajumbe wa Bodi.
11. Makamu Mwenyekiti.
12. Mikutano ya Bodi.
13. Akidi ya mikutano.

14. Maamuzi ya Bodi.

15. Taratibu za mikutano.

16. Nafasi ya mjumbe kuwa wazi.

17. Posho kwa wajumbe.

18. Mjumbe mualikwa.

19. Mgongano wa maslahi.

20. Kukasimu kazi za Bodi.

21. Kusitishwa au kusimamishwa kuwa mjumbe wa Bodi.

22. Bodi kuanzisha kamati.

**SEHEMU YA NNE**
**MKURUGENZI MKUU NA WATUMISHI WENGINE WA TAASISI**

23. Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.

24. Kazi za Mkurugenzi Mkuu.

25. Idara, vituo, divisheni na vitengo vya Taasisi.

26. Watumishi wa Taasisi.

**SEHEMU YA TANO**
**KUANZISHA KAMATI YA UTAFITI**

27. Uanzishaji na Muundo wa Kamati ya Utafiti.

28. Kazi za Kamati ya Utafiti.

**SEHEMU YA SITA**
**UENDESHAJI WA UTAFITI WA TAASISI**

29. Taarifa zinazotakiwa kuwasilishwa kwa Taasisi.

30. Masharti yanayohusiana na ugunduzi na uvumbuzi.

31. Umiliki wa ugunduzi na uvumbuzi.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA FEDHA


32. Fedha za Taasisi.

33. Makadirio ya mapato na matumizi.

34. Hesabu na ukaguzi.

35. Ripoti ya utekelezaji ya mwaka.

36. Ufunguaji wa Hesabu ya Benki.


## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI MENGINEYO


37. Makosa na adhabu.

38. Adhabu za ziada.

39. Kanuni.

40. Mipaka ya haki ya kutoa taarifa.

41. Kufuta na kubakiza.

**SHERIA NAM. 8 YA 2020**

**NIMESAINI**

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

**5 Mei, 2020**

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO ZANZIBAR NAMBA 8 YA MWAKA 2012 NA KUTUNGA SHERIA YA TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar ya 2020 na itaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na Rais.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo:

"kilimo" maana yake ni sayansi, taaluma au shughuli za kilimo, uoteshaji wa mazao, usimamizi wa maliasili katika viwango tofauti vya uandaaji na uuzaji wa bidhaa zinazozalishwa;

"utafiti wa kilimo" maana yake ni uendelezaji, ukusanyaji na ukuzaji wa taaluma ya kilimo na sayansi husika kwa kutumia mbinu za asili na uchunguzi mwengine wa kisayansi au asili katika uzalishaji, utabibu au usarifu na mfumo wa utunzaji wa mazao ya kilimo;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 6 (1) cha Sheria hii;

"zao" maana yake ni mbegu iliyopandwa au iliyojiotea wenyewe au zao la kilimo au zao lililosarifiwa;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 23 (1) cha Sheria hii;

"maradhi" maana yake ni kukosekana kwa afya ya kawaida kwa mmea kutokana na maambukizi ya vidudu, lishe duni au urithi ambao huathiri mmea na kuathiri uzalishaji wa mazao ya kilimo;

"mkulima" maana yake ni mtu anayemiliki, anayesimamia au anayelima kwa kuzingatia teknolojia za kilimo;

"Taasisi" maana yake ni Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3(1) cha Sheria hii;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya kilimo;

"Wizara" maana yake ni Wizara inayohusika na masuala ya kilimo;

"maliasili" maana yake ni maliasili za misitu kama ilivyotafsiriwa katika sheria inayohusika na usimamizi wa maliasili;

"kiumbe muharibifu" maana yake ni aina yoyote ya kiumbe kinachotokana na miti, wadudu, wanyama au viumbe hai vinavyosababisha madhara kwenye miti au mazao;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"aina" maana yake ni kundi la mimea lenye muundo wa vinasaba vya daraja la chini ambalo linaweza:

(a) kuelezewa kwa muonekano, tabia inayotokana na kinasaba husika au mchanganyiko wa vinasaba tofauti;

(b) kutofautishwa na aina nyengine ya mimea kwa kuonesha angalau moja kati ya tabia zilizoainishwa; au

(c) kuzalishwa mara kadhaa bila ya kuonesha tofauti.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA KWA TAASISI

Kuanzishwa kwa Taasisi.

**3.**-(1) Kunaanzishwa Taasisi itakayojulikana kama Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar na kwa ufupisho wake itajulikana kama "ZARI".

(2) Taasisi itakuwa ni chombo kinachojitegemea kwa baadhi ya mambo, kwa muundo na hadhi yake itakuwa na uwezo wa:

(a) kupata, kumiliki, kununua au kuhamisha mali yoyote inayohamishika au isiyohamishika;

(b) kuingia kwenye mkataba wowote, ubia au muamala kwa mujibu wa sheria;

(c) kukopa fedha kutoka katika taasisi yoyote ya kifedha kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma; na

(d) kutekeleza au kufanya jambo lolote au kitu chochote ambacho taasisi kwa aina yake inaweza kutekeleza kwa mujibu wa sheria.

Muhuri na nembo ya Taasisi.

**4.**-(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Taasisi katika umbo na namna kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo ya Taasisi katika waraka wowote ule yatathibitishwa kwa saini ya Mkurugenzi Mkuu au afisa mwengine yeyote wa Taasisi aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu.

(3) Waraka wowote unaokusudiwa kuwa ni hati inayotolewa na Taasisi utawekwa muhuri wa Taasisi na kuthibishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo (2) cha kifungu hiki.

Kazi za Taasisi.

**5.**-(1) Taasisi itaendesha, itasimamia na itaratibu shughuli zote za utafiti wa kilimo ndani ya Zanzibar.

(2) Bila ya kuathiri ujumla wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Taasisi:

(a) itafanya utafiti wa msingi wa kilimo na wa kimatokeo;

(b) itaainisha vikwazo vya uzalishaji, sera, soko, usarifu na matumizi kwenye nyanja za kilimo na itatayarisha mpango wa utafiti wa muda mfupi na mrefu kwa kuzingatia mpango mkuu wa maendeleo Zanzibar;

(c) itafanya majaribio ya shambani na maonesho ya maendeleo ya teknolojia ya kilimo au ubunifu;

(d) itaanzisha vituo mahsusi vya utafiti, vituo vidogo, maeneo ya miradi na mashamba kwenye maeneo tofauti ya kanda za kilimo ya nchi kwa ajili ya kufanya utafiti;

(e) itawafundisha maafisa wa utafiti na maafisa wa kilimo na wakulima juu ya mambo mbali mbali yanayohusiana na utafiti wa kilimo;

(f) itaandaa semina, makongamano na warsha kwenye masuala yanayohusiana na utafiti wa kilimo;

(g) itaandaa, itabuni na itafanya utafiti katika vituo na utafiti shirikishi mashambani kwa kuzingatia mipango ya maendeleo ya Zanzibar;

(h) itawapatia wadau matokeo ya utafiti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zao kikamilifu na kwa ufanisi;

(i) itachapisha matokeo ya utafiti katika jarida la utafiti, miongozo ya kilimo, waraka wa utafiti, vipeperushi na machapisho mengine yanayohusiana na utafiti na maendeleo ya kazi za Taasisi;

(j) itaanzisha na itaendeleza kituo cha kuhifadhia taarifa za utafiti wa kilimo; na

(k) itatekeleza kazi nyengine muhimu kwa madhumuni ya Sheria hii.

(3) Taasisi inaweza, katika kutekeleza kazi zake, kushirikiana na taasisi nyengine mbali mbali zinazofanana nazo ndani au nje ya Zanzibar.

## SEHEMU YA TATU
## UONGOZI WA TAASISI

Uanzishaji na Muundo wa Bodi.

**6.**-(1) Kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ambayo itaundwa na:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mkuu;

(c) Mkurugenzi anayehusika na mipango katika Wizara; na

(d) Wajumbe wengine wanne kutoka:

(i) Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar;

(ii) Taasisi ya Elimu ya Juu ya Zanzibar inayohusika na kilimo.

(iii) Jumuiya ya wakulima iliyosajiliwa; na

(iv) Jumuiya ya maliasili iliyosajiliwa.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi akiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya sayansi za kilimo, uchumi, sheria au fani nyengine zozote zinazohusiana nazo kutoka katika taasisi inayotambuliwa;

(c) ana uzoefu wa angalau miaka isiyopungua kumi katika utumishi wa umma;

(d) ana umahiri wa hali ya juu wa kusimamia kwa ufanisi na ubora majukumu ya Taasisi; na

(e) ni muadilifu.

(3) Ukitoa Mwenyekiti na wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, wajumbe wengine watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na mamlaka husika kwa kuzingatia uzoefu, utaalamu na usawa wa kijinsia.

Katibu wa Bodi.

**7.**-(1) Bodi itamteua mwajiriwa wa Taasisi mwenye sifa kuwa Katibu wa Bodi.

(2) Katibu wa Bodi atawajibika kwa Bodi na atahusika na:

(a) kuchukua kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi kwa utaratibu utakaokubaliwa na Bodi;

(b) kutunza taarifa sahihi na zenye kujitosheleza za Bodi;

(c) kuweka daftari la maamuzi ya Bodi na kuwajulisha maafisa wanaohusika;

(d) kutoa taarifa za mikutano ya Bodi kwa wajumbe;

(e) kutoa ushauri sahihi kwa Bodi pale unapohitajika; na

(f) kufanya kazi nyengine yoyote kama atakavyoelekezwa na Bodi.

Kazi za Bodi.

**8.**-(1) Bodi:

(a) itasimamia, itaelekeza, itatoa miongozo kuhusiana na majukumu ya Taasisi;

(b) itahakikisha kwamba fedha za kutosha na rasilimali zinakuwepo katika Taasisi kwa ajili ya kutekeleza malengo yake ya utafiti wa kilimo;

(c) itatoa miongozo kuhusu utayarishaji na utekelezaji wa sera za utafiti wa kilimo;

(d) itaongoza Kamati ya Utafiti katika njia nzuri ya kufikia malengo ya Sheria hii.

(e) itaajiri au itaidhinisha ajira au itamsitisha mtumishi wa Taasisi;

(f) itasimamia mali na shughuli, mapato, fedha na mambo mengine ya Taasisi;

(g) itaomba na itapokea kwa niaba ya Taasisi zawadi, michango, ada, malipo na fedha nyengine zinazolipwa kwa Taasisi na kuidhinisha matumizi yake;

(h) itatoa miongozo ya uendeshaji kwa idara zote au baadhi; na

(i) itaidhinisha miongozo inayoelezea masharti yanayohusiana na ununuzi, uuzaji, uchukuaji au utoaji wa ugunduzi wa aina yoyote.

(2) Waziri anaweza kutoa kwa Bodi miongozo halali kwa jambo la jumla au maalum kuhusiana na utekelezaji wa kazi za Taasisi chini ya Sheria hii.

Uwezo wa Bodi.

**9.** Bodi itakuwa na uwezo wa jumla wa kusimamia kuhusiana na utekelezaji wa kazi za Taasisi, na kwa mahsusi itakuwa na uwezo wa:

(a) kupendekeza muundo wa kitaasisi wa Taasisi kwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma;

(b) kupendekeza kwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma kuhusiana na taratibu na masharti ya utumishi ya watumishi wa Taasisi;

(c) kuajiri au kuteua watumishi wa Taasisi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma;

(d) kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya mtumishii yeyote kwa kosa la kuvunja maadili kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na kanuni zake; na

(e) kuidhinisha ada na tozo nyengine za huduma zinazotolewa na Taasisi.

Muda wa wajumbe wa Bodi.

**10.**-(1) Mwenyekiti wa Bodi atashika nafasi kwa kipindi cha miaka minne kutoka tarehe ya uteuzi na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine.

(2) Ukitoa mjumbe anayeingia kwa nafasi yake, wajumbe wengine wa Bodi watashika nafasi kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka terehe ya uteuzi na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine.

Makamu Mwenyekiti.

**11.** Wajumbe wa Bodi watamchagua mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Mikutano ya Bodi.

**12.**-(1) Bodi itakutana kikawaida mara moja kwa kila miezi mitatu na inaweza kukutana wakati wowote pale inapohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake chini ya Sheria hii.

(2) Mikutano yote ya Bodi itaitishwa na Mwenyekiti.

(3) Endapo Mwenyekiti hayupo, Makamu Mwenyekiti ataitisha mkutano wa Bodi.

(4) Endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe waliohudhuria watamchagua mmoja miongoni mwao kuendesha mkutano, na mjumbe aliyechaguliwa atakuwa na uwezo na atatekeleza majukumu yote ya Mwenyekiti.

Akidi ya mikutano.

**13.** Zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe wataunda akidi ya mkutano wa Bodi.

Maamuzi ya Bodi.

**14.** Bodi itatoa maamuzi kwa maafikiano na ikitokezea kutokukubaliana, uamuzi utafikiwa kwa kura na ikitokezea kura kuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

15. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kuandaa taratibu zake yenyewe kuhusiana na mikutano na utaratibu wa kutekeleza majukumu yake ikijumuisha kamati za Bodi.

Taratibu za mikutano.

16. Nafasi ya mjumbe wa Bodi itakuwa wazi ikiwa mjumbe huyo:

Nafasi ya mjumbe kuwa wazi.

(a) amefariki;

(b) ameshindwa kuhudhuria mikutano mitatu mfululizo ya Bodi bila ya sababu ya msingi;

(c) amejiuzulu au kwa namna yoyote amepoteza sifa **ya** ujumbe wa Bodi; au

(d) ameshindwa kutekeleza majukumu yake kwa sababu ya afya ya kimwili au kiakili.

17. Mwenyekiti na wajumbe wa Bodi watastahiki kulipwa posho kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

Posho kwa wajumbe.

18. Bodi inaweza kumualika mtu yeyote ambaye sio mjumbe kuhudhuria katika majadiliano ya mkutano wa Bodi kama mtaalamu lakini mtu huyo aliyealikwa hatokuwa na haki ya kupiga kura.

Mjumbe mualikwa.

19. Mjumbe yeyote ambaye ana maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo katika mkataba au mapendekezo ya mkataba au jambo lolote linalojadiliwa na Bodi, atatangaza uhalisia wa maslahi yake kwa Bodi na ataondoka katika ushiriki wa majadiliano ya jambo hilo.

Mgongano wa maslahi.

20. Bodi inaweza, inapoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Mkurugenzi Mkuu, kamati yoyote au mtumishi mwengine wa Taasisi.

Kukasimu kazi za Bodi.

21. Waziri anaweza kumsitisha au kumsimamisha mjumbe yeyote wa Bodi isipokuwa Mwenyekiti na Mjumbe anayeingia kwa nafasi yake ikiwa mjumbe huyo:

Kusitishwa au kusimamishwa kuwa mjumbe wa Bodi.

(a) hawezi kutekeleza kazi za nafasi yake;

(b) ametiwa hatiani kwa kosa la jinai linalohusisha udanganyifu, kutokuwa mwadilifu au uvunjifu wa maadili; au

(c) ameshindwa kuhudhuria katika mikutano mitatu mfululizo ya Bodi bila ya ruhusa ya Mwenyekiti.

Bodi kuanzisha kamati.

**22.**-(1) Bodi inaweza, kwa madhumuni ya kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake, kuanzisha kamati kwa ajili ya kutekeleza kazi maalum pale inapoona inafaa.

(2) Taratibu, masharti na mambo mengine yanayohusiana na kamati zinazoanzishwa zitaelezwa na Bodi.

## SEHEMU YA NNE
## MKURUGENZI MKUU NA WATUMISHI WENGINE WA TAASISI

Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.

**23.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya pili katika fani ya kilimo au elimu yoyote inayohusiana na sayansi kutoka katika taasisi yoyote inayotambulika;

(c) ana uzoefu katika utumishi wa umma usiopungua miaka kumi katika fani hiyo; na

(d) ni muadilifu.

Kazi za Mkurugenzi Mkuu.

**24.**-(1) Mkurugenzi Mkuu atakuwa Afisa Mtendaji Mkuu na atatekeleza kazi za kila siku za Taasisi.

(2) Bila ya kuathiri ujumla wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi Mkuu:

(a) ataongoza Taasisi katika kupanga na kutekeleza kazi za utafiti wa kilimo kwa ajili ya maendeleo;

(b) atasimamia fedha na rasilimali nyengine za Taasisi;

(c) atawezesha utekelezaji wa programu za utafiti na tathmini zake;

(d) atakuwa ni mamlaka ya kinidhamu kwa watumishi wa Taasisi walioko kwenye mamlaka yake; na

(e) atatekeleza kazi nyengine zozote kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria hii.

Idara, vituo, divisheni, na vitengo vya Taasisi.

**25.**-(1) Kwa madhumuni ya utekelezaji mzuri wa kazi za Taasisi chini ya Sheria hii, Bodi inaweza kuanzisha idara, vituo, divisheni na vitengo, kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, wakuu wa idara, vituo, divisheni na vitengo watateuliwa na Bodi kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(3) Wakuu wa idara, vituo, divisheni na vitengo watawajibika chini ya Mkurugenzi Mkuu.

Watumishi wa Taasisi.

**26.** Taasisi, kwa idhini ya Bodi na kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, itaaajiri watumishi wengine kama itakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi za Taasisi.

## SEHEMU YA TANO
## KUANZISHA KAMATI YA UTAFITI

Uanzishaji na Muundo wa Kamati ya Utafiti.

**27.**-(1) Kutakuwa na Kamati ya Utafiti itakayojulikana kama Kamati ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar ambayo itaundwa na:

(a) Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ambaye atakuwa ni Mwenyekiti;

(b) Wakurugenzi wa idara wa Taasisi;

(c) Mkurugenzi anayehusika na maliasili; na

(d) Mkurugenzi anayehusika na kilimo.

(2) Kamati ya Utafiti inaweza kumualika mtu yeyote kusaidia katika utekelezaji wa kazi zake.

(3) Kamati ya Utafiti itamteua afisa mwenye sifa miongoni mwa watafiti wa Taasisi kuwa Katibu wa Kamati ya Utafiti.

Kazi za Kamati ya Utafiti.

**28.** Kamati ya Utafiti:

(a) itaandaa mipango kazi ya mwaka ya Taasisi na kuiwasilisha kwa Bodi;

(b) itapitia mapendekezo ya miradi ya utafiti kwa kuzingatia vipaumbele na utaalamu na kuiwasilisha kwa Bodi;

(c) itapitia nyaraka za kisayansi katika utafiti wa kilimo kwa kupata idhini ya Bodi kwa ajili ya kuchapishwa;

(d) itaandaa mkutano wa mwaka wa mapitio ya tafiti za kilimo, semina na makongamano kwa wadau;

(e) itafuatilia na kutathmini maendeleo ya utafiti na kuwasilisha matokeo yake kwa Bodi; na

(f) itafanya kazi nyengine zozote zitakazoelezwa au kuelekezwa na Bodi.

## SEHEMU YA SITA
## UENDESHAJI WA UTAFITI WA TAASISI

Taarifa zinazotakiwa kuwasilishwa kwa Taasisi.

**29.** Mtu yeyote anayetaka au anayekusudia kufanya utafiti wa kilimo ndani ya Zanzibar, kwa gharama zake, atatoa taarifa kwa Taasisi kuhusiana na utafiti huo, na atawasilisha kwa Taasisi nakala za kumbukumbu zozote husika na matokeo ya utafiti huo.

Masharti yanayohusiana na ugunduzi na uvumbuzi.

**30.**-(1) Kwa madhumuni ya matumizi ya kibiashara kwa ugunduzi au uvumbuzi wowote ambao Taasisi inaona ni muhimu kutumia kwa ajili ya uendelezaji wa uzalishaji wa kilimo, Taasisi inaweza kukubaliana na mtu yeyote kununua, kuuza, kuchukua au kutoa ugunduzi wowote unaohusiana na kilimo kwa kuzingatia utaratibu na masharti yaliyoidhinishwa na Bodi.

(2) Ugunduzi au uvumbuzi uliofanywa ikiwa ni matokeo ya utafiti uliofanywa chini ya Sheria hii, utasajiliwa na Taasisi katika namna na masharti ambayo Waziri anaweza kuyaweka katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

Umiliki wa ugunduzi na uvumbuzi.

**31.**-(1) Ugunduzi na uvumbuzi wowote unaohusiana na kilimo uliofanywa na Taasisi katika utekelezaji wa kazi zake chini ya Sheria hii, utakuwa ni miliki ya Taasisi na Taasisi inaweza kuuweka wazi kwa umma.

(2) Taasisi inaweza, kwa idhini ya Waziri:

(a) kutoa tunzo au mrabaha kama itakavyoona inafaa, kwa mtu yeyote ambaye amefanya ugunduzi au uvumbuzi kutokana na utafiti wowote uliofanywa, au ulioelekezwa kufanywa na Taasisi, ama mtu huyo ni mwajiriwa wa Taasisi au vyenginevyo; na

(b) endapo ugunduzi au uvumbuzi umewekwa wazi kwa umma kwa malipo au mrabaha, kumsamehe mtu yeyote kutolipa ada au mrabaha au sehemu yake.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha za Taasisi.

**32.**-(1) Fedha na rasilimali za Taasisi zitajumuisha:

(a) fedha zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi katika mfumo wa ruzuku;

(b) fedha zilizopokelewa na Taasisi kutokana na bidhaa au huduma zilizotolewa na Taasisi;

(c) misaada halali, zawadi, michango, mikopo, urithi, au uwekezaji kama Taasisi itakavyopokea kutoka kwa mtu yeyote au taasisi; na

(d) fedha nyengine zozote itakazopewa au kupatikana kihalali na Taasisi kutokana na utekelezaji wa kazi zake au vyenginevyo.

(2) Taasisi itatekeleza kazi zake kwa mujibu wa misingi ya jumla ya fedha na itahakikisha kwamba, kadri iwezekanavyo, makusanyo yake yanatosheleza matumizi yake sahihi kwa mujibu wa mpango mkakati.

(3) Waziri anaweza, baada ya kushauriana na waziri anayehusika na fedha, kuamua kiwango cha makusanyo ambacho kitabakia kuwa mali ya Taasisi na kiwango cha makusanyo ambacho kitachukuliwa kuwa ni fedha za umma na kuwasilishwa katika hesabu ya Serikali.

(4) Miamala yote ya fedha ya Taasisi itafanywa na itaongozwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na sheria nyengine yoyote ya fedha.

Makadirio ya mapato na matumizi.

**33.**-(1) Mkurugenzi Mkuu, katika kila mwaka wa fedha, atawasilisha kwa Bodi ya Wakurugenzi kwa majadiliano na mapendekezo, makadirio ya mapato na matumizi kwa ajili ya Taasisi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Kutokana na majadiliano na mapendekezo ya Bodi, bajeti ya Taasisi itafanywa katika namna ile ile ikiwa ni sehemu ya Bajeti ya Wizara.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, makadirio ya mapato na matumizi yanaweza yakajumuisha makadirio ya ziada.

(4) Makadirio ya mapato na matumizi ya Taasisi yataandaliwa kwa mujibu wa masharti na taratibu za Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na miongozo mengine yoyote itakayotolewa na Serikali mara kwa mara.

(5) Mkurugenzi Mkuu atahakikisha kwamba malipo yote yanayofanywa na fedha za Taasisi yanafanywa kwa usahihi na yanaidhinishwa ipasavyo, na udhibiti unaopaswa unazingatiwa kwa mali na madeni ya Taasisi.

Hesabu na ukaguzi.

**34.**-(1) Taasisi itawezesha kufanywa na kuwekwa vitabu sahihi na kamili vya hesabu vinavyoainisha mapato yote na matumizi ya Taasisi.

(2) Mkurugenzi Mkuu, kwa kuzingatia miongozo ya Taasisi, ataandaa kuhusiana na uendeshaji wa Taasisi, katika kila mwaka wa fedha, taarifa za hesabu ambazo zinajumuisha:

(a) taarifa ya fedha na taarifa ya mapato na matumizi; na

(b) taarifa nyenginezo zinazohusiana na mambo ya fedha za Taasisi kama inavyotakiwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

(3) Ndani ya miezi mitatu ya ufungaji wa kila mwaka wa fedha, hesabu zitakazojumuisha taarifa za fedha za Taasisi zinazohusika na mwaka wa fedha huo, zitawasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Ripoti ya utekelezaji ya mwaka.

**35.**-(1) Mkurugenzi Mkuu, ndani ya miezi miwili baada ya kila mwisho wa mwaka wa fedha, ataandaa na kuwasilisha kwa Waziri ripoti ya utekelezaji ya mwaka kuhusiana na mwaka huo wa fedha, itakayojumuisha:

(a) nakala ya hesabu zilizokaguliwa za Taasisi, pamoja na ripoti ya ukaguzi kuhusiana na hesabu hizo;

(b) ripoti ya Taasisi ya mwaka wa fedha huo; na

(c) taarifa nyengine kama Waziri atakavyohitajia.

(2) Waziri atawezesha nakala ya ripoti ya utekelezaji ya mwaka ya Taasisi kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi, ndani ya miezi miwili au katika Mkutano unaofuata wa Baraza la Wawakilishi, baada ya kupokea ripoti hiyo chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

Ufunguaji wa Hesabu ya Benki.

**36.** Taasisi, kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, itafungua hesabu ya Benki na kuweka fedha zake kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi zake kwa mujibu wa Sheria hii.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI MENGINEYO

Makosa na adhabu.

**37.**-(1) Mtu ambaye:

(a) anafanya udanganyifu au ametoa taarifa isiyo sahihi ambayo inakwaza utekelezaji wa kazi za utafiti wa kilimo;

(b) anaingilia katika ufanyaji wa utafiti wa kilimo;

(c) anamzuia au anamkwaza afisa utafiti wa kilimo katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii;

(d) anahaulisha matokeo ya utafiti wake pahala pengine kwa njia ya siri;

(e) ameshindwa kufuata masharti ya kifungu cha 29 cha Sheria hii; au

(f) anaathiri au anaharibu mali au kazi yoyote ya utafiti wa kilimo uliofanywa chini ya Sheria hii,

atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja lakini isiyozidi Shilingi za Kitanzania Milioni Kumi au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka kumi au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

Adhabu za ziada.

**38.** Mtu yeyote atakapotiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria hii, Mahakama, mbali na adhabu aliyopewa chini ya Sheria hii, itaamuru:

(a) iwapo miundombinu ya utafiti au utafiti wa kilimo umeharibiwa, umeathiriwa au umeondolewa kwa dhamira ya kutenda kosa, mtu huyo atalipa fidia inayofanana na thamani ya uharibifu alioufanya; na

(b) kutaifishwa mali iliyotumika katika kutenda kosa.

Kanuni.

**39.** Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

Mipaka ya haki ya kutoa taarifa.

**40.** Isipokuwa kwa madhumuni ya mwenendo wa jinai au uendeshaji wa jinai, Taasisi ikiwa ni chombo cha Serikali haitowajibika kutoa taarifa ambazo kwa maoni ya Taasisi, itaondosha uaminifu kwenye utafiti, hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea au haki nyengine zinazohusiana nazo.

Kufuta na kubakiza.

**41.**-(1) Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar Nam. 8 ya 2012 inafutwa.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jambo lolote lililofanywa chini ya Sheria iliyofutwa litachukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 2 Aprili, 2020.

..........................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***